# MPINGA KRISTO

## Sehemu ya 3, Somo la 37



Neno lako ni kweli

– Yohana 17:17

*Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482*

# MPINGA KRISTO-3

Leo tutahitimisha somo letu kuhusu Mpinga Kristo. Baada ya kutambua kwa kutumia maandiko na kuthibitisha kwa kina kuwa mfumo wa Mpinga Kristo ni Upapa, sasa tutaona jinsi maandiko yanavyoelezea "kuzaliwa" kwake, "maendeleo" yake, na mwisho wake wa mwisho. Biblia inatoa rekodi na uelewa wa wazi kuhusu jambo hili katika kitabu cha Ufunuo sura ya 12 na 17, sura ambazo huzungumzia wanawake wawili tofauti kabisa.

**Ufunuo Sura ya 12**

**Mstari wa 1:** *"Ikaonekana ishara kubwa mbinguni; mwanamke aliyevikwa jua, na mwezi chini ya miguu yake, na taji ya nyota kumi na mbili juu ya kichwa chake" (Ufunuo 12:1).*

Bila shaka hii si kweli kwa maana halisi. Ni picha ya mfano ya ajabu ya kanisa la Kikristo la kweli katika karne ya kwanza ya enzi ya Injili, katika siku za mitume. Kanisa limeonyeshwa kama mwanamke kwa sababu linapaswa kuwa "bibi-arusi" wa Yesu. Lilikuwa na "nuru" ya maarifa ya injili ("jua") na lilikuwa limejengwa juu ya msingi wa sheria ya Agano la Kale pamoja na mifano na unabii wake ("mwezi"). Walimu waliowekwa na Mungu kwa ajili yake walikuwa mitume kumi na wawili ("nyota kumi na mbili").

***Mstari wa 2:*** *"Naye alikuwa na mimba, akalia kwa uchungu, hali ya kuzaa ikimfika" (Ufunuo 12:2)*

.

Ndani ya mwili wa kanisa maisha mapya yalianza kukua kwa siri, kama inavyokuwa ndani ya tumbo la mwanamke mjamzito. Mfumo huu wa Mpinga Kristo ambao ulianza kujitokeza ndani ya mwili wa kanisa umetajwa na mtume Yohana: "Walitoka kwetu" (1 Yohana 2:19). Kauli "akalia kwa uchungu, hali ya kuzaa ikimfika" inaonyesha huzuni miongoni mwa wanachama wa kanisa la kweli kuhusu yale yaliyokuwa yakitokea ndani yao. Hili pia linaonyeshwa katika mojawapo ya mifano ya Bwana wetu:

*"Watumwa wa yule bwana wa nyumba walimwendea, wakamwambia, Bwana, hukupanda mbegu njema katika shamba lako? Basi, magugu yamepataje kuwamo?" (Mathayo 13:27).*

Angalia huzuni ilipojitokeza wakati "magugu" yalipoonekana. Hii inaelezea hali ya kanisa la mwanzo kuanzia mwisho wa karne ya kwanza hadi karne ya pili.

***Mstari wa 3:*** *"Ikaonekana ishara nyingine mbinguni; na tazama, joka kubwa jekundu, lenye vichwa saba na pembe kumi, na vilemba saba juu ya vichwa vyake" (Ufunuo 12:3).*

Hii inaelezea mamlaka iliyokuwa ikitawala wakati huo, yaani Dola ya Kirumi. Katika muktadha huu "mbinguni" humaanisha mamlaka ya kidini juu ya watu. Dola ya Kirumi ilikuwa ni muunganiko wa mamlaka ya kiraia na ya kidini, kama zilivyokuwa tawala nyingi za kale zikiwemo Babeli, Umedi-Uajemi, na nyingine. Wafalme wa tawala hizo walijitangaza kuwa wawakilishi wa miungu yao, jambo ambalo liliwapa haki ya kuwa na mamlaka ya kidini juu ya watu. Hili liliwasaidia sana kuimarisha utawala wao wa kiraia na madai yao ya haki ya kutawala. "Joka kubwa jekundu" (yaani Dola ya Kirumi) lilikuwa "mbinguni" (katika mamlaka ya kidini) hadi takribani

mwaka 300 B.K. Alama hii ya Dola ya Kipagani ya Kirumi pia imeelezewa na Danieli:

*“Nayo ilikuwa tofauti na wanyama wengine wote waliotangulia, nayo ilikuwa na pembe kumi” (Danieli 7:7).*

“Vichwa saba” vinawakilisha aina saba za serikali zilizowahi kutawala Dola ya Kirumi. Aina nne za kwanza zilikuwa: 1) Utawala wa Makonsuli mwaka 30 K.K.; 2) Utawala wa Kifalme mwaka 27 K.K.; 3) Utawala wa Wagothi mwaka 476 B.K.; 4) Utawala wa Kipapa ulioanza mwaka 539 B.K. “Pembe kumi” zinaeleza migawanyiko kumi ya dola hiyo.

**Ufunuo 12:4** *“Mkia wake wakokota theluthi ya nyota za mbinguni, akazitupa hata nchi. Na yule joka akasimama mbele ya yule mwanamke aliyekuwa karibu kuzaa, apate kumla mtoto wake atakapozaliwa.” (SUV)*

Hii inaelezea kile kilichotokea katika kanisa la awali hadi kufikia takribani mwaka 325 B.K. “Mkia wa joka” ni sehemu ya mwisho kabisa ya mwili wake. Kwa hivyo, inawakilisha mwisho wa Dola ya Kirumi, yaani wafalme wake wa mwisho, ikimaanisha hasa mmoja wa wafalme wa mwisho—Konstantino. Kukokota “theluthi ya nyota za mbinguni” kunarejelea mkutano maalum wa maaskofu wa Kikristo (“nyota mbinguni”) ulioandaliwa na Konstantino kujadili swali kuhusu asili ya Yesu na jinsi ya kufasiri **Yohana 10:30 (“Mimi na Baba tu umoja”)**. Takriban theluthi ya maaskofu wa Kikristo wa wakati huo walikubali mwaliko wa Konstantino na kuhudhuria mkutano huo. Kauli “akazitupa hata nchi” inaonyesha athari aliyowaletea maaskofu hao. Heshima na thawabu za kidunia alizowapa ziliwavutia kiasi cha kuacha mambo ya kiroho kwa ajili ya ya kidunia. Maaskofu hawa waligeuka kuwa wa kidunia na wakaanguka kutoka kwenye nafasi yao ya juu ya kiroho. Kwa maana hiyo, “aliwatupa chini.”

Kauli "yule joka akasimama mbele ya yule mwanamke" inawakilisha mateso na upinzani alioupata "mwanamke" (kanisa) kutoka kwa "joka" (yaani Dola ya Kipagani ya Kirumi). Inaweza pia kurejelea mateso makali ya miaka kumi yaliyofanywa na Mfalme Dioklesiano wa Kirumi dhidi ya kanisa, yaliyotajwa awali katika Ufunuo:

*"Usiogope hayo utakayoyapata; tazama, ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani, ili mpate kujaribiwa, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi" (Ufunuo 2:10, SUV).*

Siku hizi kumi za kinabii ni miaka kumi halisi, kutoka mwaka 303 hadi 313 B.K.

Kauli "apate kumla mtoto wake atakapozaliwa" inatupeleka hadi mwaka 313 B.K. ambapo mfalme aliyefuata wa Kirumi, yaani Konstantino, alionekana kuwa na huruma zaidi. Alikubali "Ukristo" wa Askofu wa Roma na yeye mwenyewe akawa Mkristo. Askofu huyu wa Roma alizidi kuwa na mamlaka na hatimaye alijulikana kama Papa—kiongozi wa mfumo wa Mpinga Kristo uitwao Upapa. Hapo ndipo Mpinga Kristo "alizaliwa" au alionekana kwa mara ya kwanza kwa namna inayoonekana. "Joka" lilimla "mtoto wake" kwa maana kwamba Dola ya Kirumi ilipokubali "Ukristo" wa Askofu wa Roma, iliukumbatia mfumo huu mchanga wa Mpinga Kristo. Hivyo, Rumi ya Kipagani ikawa "ya Kikristo" na ikajibadilisha kuwa Rumi ya Kipapa.

**Ufunuo 12:5** *"Naye akazaa mtoto mwanamume, mwenye kutawala mataifa yote kwa fimbo ya chuma. Na mtoto wake akanyakuliwa hata kwa Mungu, na kwa kiti chake cha enzi." (SUV)*

Taratiibu, mfumo huu mchanga na uliokuwa umeanza tu kuzaliwa ulibadilika na kuwa kile ambacho Paulo alikiita "mtu wa kuasi" (2 Wathesalonike 2:3). Kauli "kutawala mataifa yote kwa fimbo ya

chuma" inaelezea kwa uwazi utawala wa Upapa wakati wa Enzi za Giza. Na kusema kwamba "akanyakuliwa hata kwa Mungu, na kwa kiti chake cha enzi" kunaeleza juu ya kujitukuza kwa mfumo wa Kipapa. Kama Paulo alivyoeleza:

*"Hujikweza juu ya kila kiitwacho Mungu au kuabudiwa; hata huketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu." (2 Wathesalonike 2:4, SUV)*

**Ufunuo 12:6** *"Yule mwanamke akakimbilia nyikani, ambapo ana mahali palipotengenezwa na Mungu, ili wamlishe huko siku elfu na mia mbili na sitini." (SUV)*

Hapa mtazamo unarudi kwa "mwanamke," yaani kanisa la kweli la Yesu Kristo, na hali yake katikati ya maendeleo haya yote ya mfumo wa Mpinga Kristo. Kukimbilia "nyikani" kunaonyesha kujitenga kwa wanakanisa wa kweli na matendo na kazi za wale walio katika mfumo wa Mpinga Kristo—yaani kanisa la jina tu. Kulikuwa na wakati uliopangwa wa mfumo huu wa Mpinga Kristo kuruhusiwa kuwa na mamlaka: siku 1,260 za kinabii. Hili lilikuwa ni unabii wa wakati uliomaanisha kipindi cha miaka 1,260 halisi kuanzia mwaka 539 B.K. hadi 1799 B.K.

**Ufunuo 12:7** *"Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka. Yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake." (SUV)*

Mstari huu unarudi kuelezea kile kilichokuwa kikitokea katika kanisa la jina tu kuanzia karne ya nne hadi ya sita, yaani tangu mwaka 325 B.K. "Vita mbinguni" vinamaanisha ile "mbingu" ya mstari wa kwanza na wa tatu, **yaani ulimwengu wa kidini.** "Vita" ni ishara ya mapambano. Katika upande mmoja wa "vita" hii yuko "Mikaeli na

malaika zake." Mikaeli ni jina la Yesu mbinguni na linamaanisha "**mfano wa Mungu"** au "aliye kama Mungu." Jina hili linaashiria yule anayejidai kuwa mwakilishi wa Mungu duniani, yaani tena ni rejea kwa Upapa. "Mikaeli na malaika zake" wanawakilisha Askofu wa Roma na washiriki wengine walioasi katika kanisa ambao walitafuta mamlaka ambayo baadaye yaliunda mfumo wa Upapa. "Joka na malaika zake" wanawakilisha Dola ya Kirumi katika mamlaka yake ya kiraia na ya kidini. "Vita" hii au mapambano yalikuwa juu ya udhibiti wa "mbingu," yaani ulimwengu wa kidini au uongozi wa kidini, na mapambano haya yalikuwa ya muda mrefu.

**Ufunuo 12:8-9** *"Wala hawakuweza kushinda, wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni. Yule joka mkubwa akatupwa chini, nyoka yule wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote." (SUV)*

Baada ya mapambano ya muda mrefu kuanzia mwaka 325 B.K. hadi 539 B.K., wanakanisa walioasi chini ya uongozi wa Askofu wa Roma "walishinda" na wakapata mamlaka ya kidini kutoka kwa Rumi ya Kipagani.

"Yule joka mkubwa akatupwa chini, nyoka yule wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani." Alama ya "joka" ambayo ni ishara ya Dola ya Kirumi sasa inabadilika kuwa "Ibilisi au Shetani" kwa sababu Dola ya Kirumi ilikuwa kama Shetani katika nyanja nyingi, kama vile uwezo wake wa kubadilisha "mfumo" wa utawala wake kama Shetani anavyobadilika. Sifa nyingine za Shetani zilikuwa ndani ya Dola ya Kirumi, na hivyo jina hilo linamfaa.

"Kutupwa chini" kunaashiria kuondolewa kwa Dola ya Kirumi kutoka kwenye mamlaka ya kidini, na kuachwa tu na mamlaka ya kiraia—yaani "nchi." Maneno "mahali pao hapakuonekana tena

mbinguni" yalitokea wakati cheo cha *Pontifex Maximus* (kiongozi wa mambo yote ya kidini) kilipopitishwa kutoka mikononi mwa Dola ya Kirumi kwenda kwa Askofu wa Roma mnamo mwaka 539 B.K.

**Ufunuo 12:10-12** *Kisha nikasikia sauti kubwa mbinguni ikisema, Sasa kumekuja wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake; kwa maana ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye ambaye alikuwa akiwashitaki mbele za Mungu wetu mchana na usiku. Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa. Kwa hiyo shangilieni, enyi mbingu, nanyi mkaao ndani yake. Ole wa dunia na wa bahari! kwa maana yule Ibilisi amewashukia, mwenye ghadhabu nyingi, akijua ya kuwa ana wakati mchache tu." (SUV")*

Mistari hii inaonyesha kwa mfano wa picha uthibitisho wa nguvu wa mfumo wa Upapa baada ya mwaka 539 B.K. Mfumo huu ulithibitishwa kwa nguvu zaidi mnamo mwaka 799 B.K. kwa kuanzishwa kwa "Dola Takatifu ya Kirumi" (The Holy Roman Empire). Wakati huo madai makubwa yalitolewa na Askofu wa Roma kupitia mamlaka yake mapya alipoongea kwa "sauti kubwa" kutoka "mbinguni." Alidai: "Sasa kumekuja wokovu, na nguvu." Hii ni kauli ya Askofu wa Roma baada ya kushinda mapambano na Dola ya Kirumi na kuwa Pontifex Maximus. Kauli "ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake" inaonyesha dai la Upapa kuwa wao ni "Ufalme wa Mungu" na wanatekeleza utawala wa miaka elfu ya Kristo: "Wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu" (Ufunuo 20:4). Hivyo, Upapa ulidai kuwa na "mamlaka ya Kristo" katika utawala wao tangu mwaka 799 hadi 1799 B.K.

Kauli "kwa maana ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye ambaye alikuwa akiwashitaki mbele za Mungu wetu mchana na usiku" inahusiana na majibu ya Upapa wakati Dola ya Kirumi ilipopoteza mamlaka ya udhibiti wa kidini. Maneno "mshitaki wa

ndugu zetu" yanaelezea mateso ya Dola ya Kirumi dhidi ya kanisa kwa kipindi kirefu kabla ya tukio hilo kutokea.

"Wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa." Haya yote ni madai ya Upapa kuonyesha kuwa walipata mamlaka kwa uongozi wa kimungu. Pia inazungumzia mashahidi wa mfumo wa Upapa: "hawakupenda maisha yao hata kufa." Hakika, kulikuwa na "watakatifu" wengi waliotoa maisha yao kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza mfumo huu wa Kipapa.

"Kwa hiyo shangilieni, enyi mbingu, nanyi mkaao ndani yake." Hii inaonyesha kipindi cha utukufu na nguvu kilichokuja kwa mfumo wa Upapa kwani sasa ulikuwa "mbinguni," yaani kwenye mamlaka ya juu ya mambo ya kidini. Hii pia ilikuwa sababu ya "shangwe" kwa "ninyi mkaao ndani yake," yaani wale waliokuwa sehemu ya mfumo wa Kipapa ikiwa ni pamoja na tabaka la juu la makadinali, maskofu wakuu, maaskofu, mapadre na watawa.

"Ole wa dunia na wa bahari." Hata hivyo, "ole" ulileta na utawala wa Kipapa kwa "dunia," yaani jamii zilizoandaliwa za mataifa ya ustaarabu, na kwa "bahari," yaani mataifa ya watu wa kawaida wasio na dini (wasio na ustaarabu) ambapo Ukristo haukujulikana. "Ole" hii ilionekana katika vita vilivyopiganwa chini ya bendera ya msalaba. Vita hivi vilijulikana kama "Vita vya Msalaba" (Crusades), ambapo kwa vurugu na umwagaji damu mwingi, utawala wa Kipapa ulilazimishwa kwa watu.

Hatimaye tunasoma: "Kwa sababu Ibilisi amewashukia! Akiwa na ghadhabu nyingi kwa kuwa anajua ya kuwa ana wakati mchache." Hii huenda inahusiana na "ninyi" kama daraja la kanisa la kweli, na jinsi ambavyo shetani au Ibilisi angeanza kutumia njia za hatari na za dharura katika juhudi zake za kuliharibu kanisa.

**Ufunuo 12:13** *"Na joka alipoona ya kuwa ametupwa chini, alimwudhi mwanamke yule aliyemzaa mtoto mwanamume." (SUV) Ingawa "joka" (mamlaka za kiraia) lilipoteza mamlaka ya kiroho, lilitumiwa kwa ujanja na mfumo wa Upapa kutesa vikali "mwanamke," yaani kanisa la kweli, katika kipindi kilichojulikana kama "Inquisition" (Danieli 7:21,25).*

Hiki kilikuwa kipindi ambacho Upapa uliwatumia watawala wa kiraia wa Ulaya kama vyombo vya kutesa na kuharibu kanisa. Ilikuwa ni kipindi ambacho Wakristo wengi waliolisadiki Neno la Mungu waliuawa.

***Ufunuo 12:14*** *"Mwanamke akapewa mabawa mawili ya tai mkuu, ili aruke mpaka mahali pake penye nyika, hapo alishwe wakati na nyakati mbili na nusu wakati, mbali na uso wa yule nyoka." (SUV)*

"Mwanamke," au kanisa la kweli, alipokea ulinzi wa pekee kutoka kwa Mungu kwa kipindi cha "wakati, nyakati mbili na nusu wakati," yaani miaka 1 + 2 + ½ = miaka 3½ ya kinabii, ambayo ni kati ya mwaka 539 hadi 1799 B.K. (miaka 1,260 halisi au miezi 42 ya kinabii). "Mabawa mawili ya tai mkuu" yanawakilisha Neno la Mungu kama lilivyo katika Agano la Kale na Jipya. "Nyika" inawakilisha hali ya upweke na kujitenga. Kanisa la kweli lilijitenga na shughuli zote za mfumo wa Mpinga Kristo.

***Ufunuo 12:15-16*** *"Nyoka akatoa katika kinywa chake, nyuma ya huyo mwanamke, maji kama mto, ili kumfanya achukuliwe na mto ule. Nayo nchi ikamsaidia mwanamke, nchi ikafumbua kinywa chake, ikaumeza mto ule alioutoa yule joka katika kinywa chake." (SUV)*

Hii ni picha ya kinabii ya Mapinduzi ya Ufaransa ya karne ya kumi na nane iliyotolewa kwa lugha ya mfano. "Nyoka" anawakilisha Shetani (Mwanzo 3:13), ambaye ndiye kiongozi wa mfumo wa

Mpinga Kristo. “Maji” katika maandiko ni ishara ya kweli (Ufunuo 22:17). Shetani alibadili mbinu zake na kusababisha ukweli fulani kama “maji kama mto” kufunuliwa kuhusu upadri wa kidini na utawala wa kifalme, pamoja na haki na uhuru binafsi wa watu. Alifikiri kuwa hatua hii ingeleta mkanganyiko mkubwa na madhara kwa kanisa la kweli. Ukweli huu ulikuwa katika maandiko ya Voltaire na Jean-Jacques Rousseau kule Ufaransa, ambao wenyewe hawakuwa na imani ya kweli katika Biblia. Lakini kweli hizi (“maji kama mto”) “zilimezwa” au zilichukuliwa na “nchi,” yaani jamii ya watu. Hili lilipelekea Mapinduzi ya Ufaransa ambayo yalimaliza utawala wa Upapa mwaka 1799.

***Ufunuo 12:17*** *“Yule joka akakasirika juu ya mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao waliosalia wa mzao wake, hao wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu.” (SUV)*

Unabii huu unahitimisha kwa picha ya jinsi ambavyo Shetani, kupitia vyombo vyake vya Upapa na mamlaka za kiraia, alijaribu kutesa (“kufanya vita”) dhidi ya kanisa la kweli (linaloitwa “wazao waliosalia”) hadi mwisho wa enzi ya Injili. Hivyo basi, sura hii ya Ufunuo inatoa maelezo wazi na ya kina kuhusu kuzaliwa na kuendelea kwa mfumo wa Mpinga Kristo.

**Ufunuo Sura ya 13**

**Ufunuo 13:1** *“Kisha nikamwona mnyama akipanda kutoka baharini, mwenye pembe kumi na vichwa saba, na juu ya pembe zake taji kumi, na juu ya vichwa vyake majina ya makufuru.” (SUV)*

Hii ni picha nyingine ya Upapa kama “mnyama,” ishara ya ufalme au himaya (tazama Danieli 7). “Pembe kumi na vichwa saba” ni ishara inayojulikana ya Dola ya Kirumi (Ufunuo 12:3). Upapa ulipata

mamlaka yake kupitia tu Dola ya Kirumi. "Taji kumi juu ya pembe zake, na juu ya vichwa vyake majina ya makufuru" inawakilisha jinsi migawanyiko kumi ya Rumi barani Ulaya ("pembe kumi") ilivyokua hatua kwa hatua na kudai kuwa ni Ufalme wa Kristo au Ukristo. Hili lilikuwa ni kufuru kwa kuwa kamwe hayakuwa Ufalme wa Kristo kwa maana yoyote ile. Bali, vilikuwa ni bandia na vililitumia jina la Kristo kwa uongo.

***Ufunuo 13:2*** *"Na yule mnyama niliyemwona alikuwa mfano wa chui, na miguu yake ilikuwa kama ya dubu, na kinywa chake kama kinywa cha simba. Yule joka akampa nguvu zake, na kiti chake cha enzi, na uwezo mwingi." (SUV*)

Hii inaelezea nguvu ya Upapa au sifa za ufalme huu wa Kipapa. Kauli "alikuwa mfano wa chui" inarejelea ishara iliyotumika kwa Uyunani (tazama Danieli 7:6). Kwa namna gani ufalme wa Kipapa ulikuwa kama "chui" au Uyunani? Paulo alisema kuhusu Wagiriki: "Enyi watu wa Athene! Nawaona kwamba katika mambo yote mmekuwa watu wa dini sana" (Matendo 17:22). Vivyo hivyo, Upapa ulijionesha kuwa wa kidini sana kupitia watawa wake, maisha ya kujitenga ya watawa na ibada za heshima zilizofanywa na mapadre na watawa.

Kauli "miguu yake ilikuwa kama ya dubu" inarejelea ishara iliyotumika kwa Umedi-Uajemi (tazama Danieli 7:5). Waajemi walijulikana sana kwa mbinu zao za kuzingira na uvumilivu, pamoja na mikakati yao. Mfumo wa Upapa ulitumia mbinu kama hizo kwa ajili ya "miguu" yake ya kupata na kudumisha mamlaka katika karne nyingi, na kuweka "msimamo" wake.

Alikuwa na "kinywa kama kinywa cha simba" ambayo ni ishara iliyotumika kwa Babeli (tazama Danieli 7:4). Babeli ilijulikana kwa ukuu na utukufu wake: "Ukuu wako umeongezeka hata kufikia

mbinguni, na mamlaka yako imeenea mpaka miisho ya dunia" (Danieli 4:22). "Kinywa" cha Upapa kilijaa madai ya ukuu na utukufu.

Kauli "yule joka akampa nguvu zake, na kiti chake cha enzi, na uwezo mwingi" ni picha ya mfano ya jinsi Upapa ulivyopokea nguvu kutoka kwa "joka," yaani Dola ya Kipagani ya Kirumi kupitia kwa Wafalme Konstantino na Justiniani. Nguvu kuu ilikuwa ni cheo cha *Pontifex Maximus,* yaani kiongozi wa mambo ya kiroho katika Dola ya Kirumi.

***Ufunuo 13:3*** *"Na moja ya vichwa vyake vilikuwa kana kwamba vimejeruhiwa hata kufa; na jeraha lake la mauti lilipona. Nao wanadamu wote wakastaajabu, wakamfuata yule mnyama." (SUV)*

"Jeraha la mauti" linaonyesha athari ya pigo la Matengenezo (Reformation) dhidi ya Upapa. Kauli inayosema "jeraha lake la mauti lilipona" inaonyesha jinsi Upapa ulivyopona kutokana na mapigo ya Matengenezo ya mwaka 1517 B.K. na kuendelea baada ya waasisi wa mageuzi kufariki. Wafuasi wao waliingia katika "roho" ile ile ya kuiunganisha makanisa yao na serikali. Hatimaye, katika karne zilizofuata, hapakuwa tena na "kupinga" kwa maana ya Matengenezo dhidi ya mfumo wa Upapa. Mfano mmoja ni Kanisa la Kilutheri kule Ujerumani lililopokea na kukubali heshima na neema kutoka kwa wafalme wa Ujerumani.

Mfano wa Upapa kama "mnyama," yaani serikali ya kanisa-serikali au himaya, unaonekana kwa wazi zaidi katika Ufunuo sura ya 17 ambayo tutaiangalia baadaye.

**Ufunuo Sura ya 17**

**Ufunuo 17:3-6** *"Kisha akanichukua katika roho mpaka jangwa; nikamwona mwanamke ameketi juu ya mnyama mwekundu sana, mwenye majina ya makufuru, mwenye vichwa saba na pembe kumi.*

*Mwanamke yule alikuwa amevaa nguo za rangi ya zambarau na nyekundu, amepambwa kwa dhahabu na vito vya thamani na lulu, alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi mwake kilichojaa machukizo, na mambo machafu ya uasherati wake; na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa,* SIRI, BABELI MKUU, MAMA WA MAKAHABA, NA MACHUKIZO YA NCHI. *Nikamwona yule mwanamke amelewa kwa damu ya watakatifu, na kwa damu ya mashahidi wa Yesu." (SUV)*

Mwanamke huyu ndiye mtesaji wa watakatifu wa Mungu, na jina lake ni **Babeli Mkuu**. Alikuwa ameketi juu ya "mnyama mwekundu sana



… mwenye majina ya makufuru, mwenye vichwa saba na pembe kumi." Isaya anaongelea kuhusu "nyekundu": *"Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji."* (Isaya 1:18). "Mnyama" anawakilisha himaya au ufalme, na "rangi nyekundu" inaashiria dhambi—hivyo hii ni picha ya **himaya ya dhambi**. Kwa hakika, ni "mtu wa kuasi," mfumo wa Mpinga Kristo wa Upapa (2 Wathesalonike 2:3-4). Kuwa "amejaa majina ya makufuru" kunaonyesha vyeo vya kufuru vinavyotumika na mfumo wa Upapa. "Vichwa saba na pembe kumi" vinathibitisha zaidi kuwa "mnyama" huyu ni Upapa, ambaye chanzo chake cha nguvu kilitoka kwa Dola ya Kirumi.

Katika Biblia, "mwanamke" mara nyingi ni mfano wa **kanisa**. Kanisa la kweli linaelezewa kama "bikira safi" (2 Wakorintho 11:2). Mwanamke huyu pia ni kanisa, lakini ni lile lililoketi juu ya "mnyama mwekundu," yaani linalopata msaada na nguvu kutoka kwa Upapa.

Hili ni **Kanisa Katoliki la Kirumi**. “Kirumi” katika jina lake linaonyesha asili yake. Hili si kanisa la Yesu Kristo; ni kanisa la Upapa, ambalo kiongozi wake ni Papa. Mwanamke huyu alivaa “zambarau na nyekundu,” ishara ya kifalme kwa kuwa kanisa hili lilitawala kwa utukufu kama sehemu ya mfumo wa “mtu wa kuasi.” “Kikombe cha dhahabu mkononi mwake” kinawakilisha “chombo” cha mafundisho ya kiungu (tazama Isaya 52:11). Kikombe cha dhahabu ni Biblia. Lakini katika kesi hii, “kikombe” hicho kilikuwa “kimejaa machukizo na mambo machafu ya uasherati wake,” kikiwa ni ishara ya jinsi Biblia ilivyodaiwa kuwa msingi wa mafundisho na matendo yote, hata yale ya uongo. Mfano mmoja ni dai la uongo kuwa ni **Ufalme wa Mungu duniani**, kama ilivyotabiriwa: *“Sasa umekuja … ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake”* (Ufunuo 12:10).

Maelezo yanaendelea: *“**SIRI, BABELI MKUU, MAMA WA MAKAHABA NA MACHUKIZO YA NCHI”*** (Ufunuo 17:5). Ishara ya “Babeli” inarejelea Mnara wa Babeli ambao wakati huo ulidaiwa kuwa ni “lango la mbinguni,” lakini uliishia kuleta mchanganyiko wa lugha. Vivyo hivyo, **Kanisa Katoliki la Kirumi** limehusika na mchanganyiko mkubwa wa mafundisho na imani zisizopatikana katika Biblia, ikiwa ni pamoja na imani kwamba Maria na watakatifu wengine wanapaswa kuabudiwa, fundisho la jehanamu ya mateso ya milele, toharani (purgatory), na fundisho la kwamba mapapa hawawezi kukosea (infallibility).

**Yeye ni “Mama wa Makahaba.”** Kanisa Katoliki la Kirumi linajulikana sana kama “kanisa mama.” “Uasherati” ni neno linaloelezea ukosefu wa uaminifu wa kiroho wa kile kinachodaiwa kuwa “Kanisa la Kristo,” ambacho badala ya kumngoja “bwana arusi” (Mathayo 25:6) na “karamu ya harusi ya Mwana-Kondoo” (Ufunuo 19:7), hujichafua kwa kujiunga na serikali za kiraia, jambo linaloitwa “**urafiki na dunia”** (Yakobo 4:4). Hili si kanisa tu lililoingia katika

uasherati wa kiroho, bali lina "binti" ambao pia ni makahaba wa kiroho. Haya ni makanisa mengine yaliyohusishwa kwa namna hiyo na miungano ya kidunia. Kwa mfano, **Kanisa la Uingereza** lilijitenga kutoka Kanisa Katoliki la Kirumi wakati wa utawala wa Mfalme Henry wa VIII mnamo mwaka 1534 na kuunda **Kanisa la Episcopali**. Kanisa hilo likawa tu mnyama mwingine wa aina ya kanisa-serikali.

Baada ya mwaka 1517 na kipindi cha Matengenezo (Reformation) yakaja makanisa ya wapinga (protestanti) kupitia kwa waasisi kama **Martin Luther, John Wesley, John Knox, John Calvin, Huldrych Zwingli**, na wengine. Ukweli wa baadhi ya maandiko ulifufuliwa na Kanisa Katoliki la Kirumi lilikemewa na hata kutambuliwa kuwa Mpinga Kristo. Lakini karne kadhaa baada ya Matengenezo, wafuasi wa waasisi hao walianza kusahau kweli hizo zilizoonyeshwa na kuiga roho ya "kanisa mama" kwa kutafuta mamlaka ya kidunia kupitia ushirikiano na serikali.

Isaya anatoa unabii wa ajabu:

*"Siku hiyo wanawake saba watamshika mtu mmoja, wakisema, tutakula chakula chetu wenyewe, na kuvaa mavazi yetu wenyewe; lakini na tuitwe kwa jina lako, utuondolee aibu yetu." (Isaya 4:1).*

"Wanawake" (wingi) wanawakilisha makanisa, tofauti na kanisa la kweli ambalo mara nyingi hurejelewa kama "mwanamke" (umoja). "Wanawake saba" wanawakilisha jumla ya makanisa yote ya uongo yaliyokuja katika hatua saba za enzi ya Injili. Wanamshika "mtu mmoja," Yesu Kristo; wote wanataka kuitwa kwa jina lake, yaani kuwa makanisa ya Kikristo. Lakini wanataka "kula chakula chao wenyewe," yaani mafundisho yao wenyewe ambayo si ya Kristo bali ya dunia. Wanataka "kuvaa mavazi yao wenyewe" badala ya kuvaa "vazi la haki" lililotolewa (Isaya 61:10). Wameshindwa kutambua kuwa haki yao wenyewe inafanana na "nguo chafu" (Isaya 64:6).

Kufanya “matendo mema” ya aina yoyote hakuwezi kufuta dhambi. Hayo hayawezi kumfanya mwenye dhambi kuwa mwenye haki. Haki ya Mkristo ni “damu ya Kristo” peke yake, na haihitaji matendo ya ziada. Hivyo basi, “wanawake” hawa ni picha ya makanisa ya Kipagani ya Kiprotestanti pamoja na Kanisa Katoliki la Kirumi.

***Kanisa la kweli*** *ni “wale wasiojitia unajisi kwa wanawake, kwa maana ni mabikira. Hawa ndio wamfuatao Mwana-Kondoo kila aendako.” (Ufunuo 14:4).*

Hawa ni wale 144,000 – washiriki wa kanisa la kweli. Kusema hawakujitia unajisi kwa wanawake kunamaanisha kuwa walipojifunza kweli, hawakuendelea kuhusiana na “wanawake,” yaani makanisa ya uongo na mafundisho yao ya uongo. *“Walijitunza safi”* inaonyesha mafundisho yao na roho ya Kristo ndani yao; wanapenda, kuamini, na kutii kweli.

Baadaye katika Ufunuo tunasoma:

*“Nikaziona roho za wale waliokatwa vichwa kwa ushuhuda wa Yesu, na kwa ajili ya neno la Mungu, na wale ambao hawakumwabudu yule mnyama, wala sanamu yake, wala kupokea chapa katika vipaji vya nyuso zao, au katika mikono yao.”* (Ufunuo 20:4).

Wajumbe wa kanisa la kweli hawatakuwa na “alama” yoyote inayohusiana na “mnyama” wala “sanamu ya mnyama.” “Alama” hii ilikuwa iwe kwenye “vipaji vya nyuso,” yaani akili zao ambako mafundisho na imani hukubaliwa, au kwenye “mikono yao,” yaani mahali ambapo msaada wa kifedha hutolewa kwa mfumo huo. Wana wa kanisa la kweli, mara tu wanapojifunza kweli, huacha mara moja msaada wowote wa kiakili au wa kifedha waliokuwa wakitoa kwa makanisa ya uongo.

***"Mnyama" huipa uhai "sanamu ya mnyama"***: *"Akapewa kutia pumzi katika sanamu ya mnyama, hata sanamu ya mnyama ikawa na roho, ikasema, na kuwafanya wote ambao hawakuiabudu sanamu ya huyo mnyama wauawe." (Ufunuo 13:15).*

"Mnyama" ni rejea ya Upapa na Kanisa Katoliki la Kirumi. "Sanamu ya mnyama" inarejelea juhudi za makanisa ya Kiprotestanti kuwa kama Upapa katika umoja na mamlaka. Ni mwili mmoja wa kimataifa. Juhudi hizi za kuungana zimepita katika hatua tatu:

1. **Muungano wa Kiinjili wa mwaka 1846** uliozalisha Shirikisho la Makanisa ya Kiprotesti.
2. 
   **2. Baraza la Makanisa Duniani mwaka 1948.**
   **3. Katika nyakati zetu, Vuguvugu la Umoja wa Kiekumene** (Ecumenical Movement) linalolenga kuleta muungano kamili wa makanisa yote ya Kiprotesti.

Sanamu hii hupokea uwezo wa "kunena." "Uwezo" huu ni mamlaka ambayo kanisa linaweza kudai kuwa ni sehemu ya kanisa la asili la Kristo tangu siku za mitume. Ni **Kanisa Katoliki la Kirumi** na **Kanisa la Uingereza** pekee ndilo linalodai kuwa na "mamlaka" haya, yanayojulikana kama *Ufuatano wa Mitume* (Apostolic Succession), unaodaiwa kuanza hasa na mtume Petro. Muungano wowote wa makanisa yote ya Kiprotesti unahitaji "idhini ya kitume" ili kutambuliwa na kuheshimiwa, na idhini hiyo huenda ikatoka kwa **Kanisa la Uingereza.** Hili likitokea, basi "binti" watakuwa katika muungano na "mama."

*"Na huyo mnyama aliyekuwako, wala hayuko sasa, ndiye mfalme wa nane. Naye ni mmoja wa wale saba, naye aenda zake kwenye maangamizi. Na zile pembe kumi ulizoziona ni wafalme kumi, ambao hawajapokea ufalme bado; lakini watapokea mamlaka kama wafalme kwa saa moja pamoja na yule*

*mnyama. Hao wana shauri moja, nao wampa yule mnyama nguvu zao na mamlaka yao."* (Ufunuo 17:11-13)

Huyu "mfalme wa nane" ni rejea kwa mfumo wa Mpinga Kristo ambaye alikuwa mmoja wa "wale saba" yaani, alikuwa miongoni mwa vichwa saba vya Dola ya Kirumi ya kale. Atakuwa "wa nane" kwa maana atapewa tena mamlaka kwa muda, lakini si kama yale aliyokuwa nayo kati ya mwaka 539 hadi 1799, kipindi cha "siku" 1,260. "Pembe kumi" ni zile zile zilizokuwa juu ya joka katika Ufunuo 12, zikimaanisha "migawanyiko kumi" ya Dola ya Kirumi. Leo hii "pembe kumi" hizi ni **mataifa ya Ulaya** ambayo yamekuwa na "nia moja" katika kitu kinachoitwa **Umoja wa Ulaya (EU).** Mipaka yao imeondolewa na hata sarafu zao zimeunganishwa kuwa **euro.**

Wafalme hawa kumi watamkabidhi mnyama nguvu na mamlaka yao. Hili litatokea wakati "pembe kumi" (Umoja wa Ulaya) zitatoa msaada kamili kwa Upapa na Kanisa Katoliki la Kirumi. Hapo ndipo **mgogoro wa mwisho** utafuata:

*"Hao watafanya vita na Mwana-Kondoo, naye Mwana-Kondoo atawashinda, kwa maana ni Bwana wa mabwana, na Mfalme wa wafalme; nao walio pamoja naye ni walioitwa, na wateule, na waaminifu."* (Ufunuo 17:14)

*"Kisha nikamwona yule mnyama, na wafalme wa dunia, na majeshi yao, wamekusanyika ili kufanya vita na yeye aliyepanda farasi, na majeshi yake."* (Ufunuo 19:19)

Hii ni picha ya **mgogoro wa mwisho** kati ya Mpinga Kristo ("mnyama," mfumo wa Upapa) na "wafalme wa dunia," yaani nguvu za kisiasa, pamoja na "majeshi yao," yaani wafuasi wa mfumo wa Upapa miongoni mwa wanadamu.

Muungano huu umeelezewa zaidi:

*"Nikaona pepo watatu wachafu mfano wa vyura, wakitoka katika kinywa cha yule joka, na katika kinywa cha yule mnyama, na katika kinywa cha yule nabii wa uongo. Hao ni roho za mashetani, watendao ishara, ambao hutoka kwa wafalme wa dunia yote, kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi."* (Ufunuo 16:13-14)

Muungano huu unajumuisha:

- **"Mnyama"** (mfumo wa Upapa na Kanisa Katoliki)
- **"Joka"** (mamlaka za kiraia za duniani)
- **"Nabii wa uongo"** (Muungano wa makanisa ya Kiprotesti wanaodai kuwa ni manabii wa Neno la Mungu lakini wanafundisha mafundisho ya uongo)

Muungano huu utajaribu kutawala dunia na kupigana na Mwana-Kondoo, **"yeye aliyepanda farasi"** (Ufunuo 19:19). **Farasi** ni mfano wa kweli safi ya Neno la Mungu, na **mpandaji** wake ni Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye ni **Neno hai.**

Je, mamlaka ya wanadamu yanawezaje kupigana na Yesu asiyeonekana? Hili linatokea wanapowapinga wajumbe wa kanisa la kweli ambao ni "viungo vya mwili" wa Mwana-Kondoo. Kutakuwa na **mgogoro wa mwisho** kati ya washiriki wa mwisho wa kanisa walioko katika mwili na mfumo wa Mpinga Kristo, sawa na jinsi Yesu alivyoingia katika mgogoro wa mwisho na mfumo wa kidini wa Kiyahudi katika siku zake.

*"Ndipo yule asiye na sheria atafunuliwa, ambaye Bwana Yesu atamwua kwa pumzi ya kinywa chake, na kumharibu kwa mafunuo ya kuja kwake."* (2 Wathesalonike 2:8)

"Asiye na sheria" au mfumo wa Mpinga Kristo **utafunuliwa**. "Siri ya kuasi" itafichuliwa na kuwekwa wazi. Hili litatimizwa kupitia

"pumzi ya kinywa cha Bwana," yaani ushuhuda na maungamo kutoka kwa "viungo wa mwisho" vya mwili wa Kristo, ambao wataufichua mfumo wa Mpinga Kristo kwa uwazi.

Hii itasababisha **uangamizi wa mwisho wa mfumo wa Mpinga Kristo**:

*"Na yule mnyama na zile pembe kumi ulizoziona watamchukia yule kahaba, nao watamfanya kuwa mgumu na uchi, wakale nyama yake, wakamteketeza kabisa kwa moto."* (Ufunuo 17:16)

Hii inaondoa msaada ambao mfumo wa Upapa ulikuwa unapata kutoka kwa "pembe kumi" na kusababisha kusambaratika kwa mamlaka na nguvu zilizoshirikiwa kati ya Upapa na nguvu za kiraia:

*"Na mji ule mkubwa ukagawanyika sehemu tatu."* (Ufunuo 16:19)

"Mji mkuu" unawakilisha **muungano wa "mnyama," "joka," na "nabii wa uongo."** Muungano huu utaanguka kabisa. Kumwacha "uchi" ni ishara ya kuvuliwa mamlaka na heshima ambayo zamani ilitolewa kwa ajili ya kumsaidia. Mamlaka za kiraia zitaanza kujiweka mbali na kujitenga na mfumo wa Mpinga Kristo mara watakapogundua kuwa kwa kweli ni "kahaba."

**"Nao watakula nyama yake"** inaonyesha jinsi mfumo mzima wa kanisa hili utakavyomezwa kabisa—yaani kuangamizwa kikamilifu. **"Nao watamteketeza kwa moto"** ni picha ya hukumu za kisasi na "ghadhabu" ya Mungu ambayo itauharibu kabisa mfumo huu:

*"Huyo naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu, iliyotiwa katika kikombe cha hasira yake pasipo kuchanganywa na maji; naye atateswa kwa moto wa kiberiti mbele ya malaika watakatifu na mbele ya Mwana-Kondoo."* (Ufunuo 14:10)

Hii inaonyesha **mateso ya kiakili** ambayo yatakumba washiriki wote wa mifumo hiyo ya uongo.

*"Kisha malaika mmoja mwenye nguvu akainua jiwe kama jiwe kubwa la kusagia, akalitupa baharini, akisema, Kwa nguvu kama hii Babeli, mji ule mkuu, utatupwa chini, wala hautaonekana tena kabisa."* (Ufunuo 18:21)

Hii ndiyo **mwisho wa mwisho wa uharibifu wa mfumo wa Mpinga Kristo**. Na kuna zaidi:

*"Yule mnyama akakamatwa, na yule nabii wa uongo pamoja naye, aliyekuwa akifanya mbele yake ishara zile alizowadanganya kwa hizo wale waliopokea chapa ya yule mnyama, na wale walioliabudu sanamu yake. Hawa wawili wakatupwa hai, katika lile ziwa la moto linalowaka kwa kiberiti."* (Ufunuo 19:20)

**"Mnyama"** anawakilisha mfumo wa kisiasa na kidini wa Upapa wa Kanisa Katoliki la Kirumi.
**"Nabii wa uongo"** ni muungano wa madhehebu mbalimbali ya Kiprotestanti—walimu wa uongo wa Neno la Mungu. Yeremia alisema kuhusu wao:

*"Manabii wanatabiri uongo kwa jina langu. Sikutuma wala kuwaagiza wala kusema nao; wanawatabiria maono ya uongo, na uchawi, na ubatili, na udanganyifu wa mioyo yao wenyewe."* (Yeremia 14:14)

Kauli **"wakatupwa hai"** inaonyesha kwamba mifumo hii bado itakuwa hai na inafanya kazi kikamilifu wakati itakapotupwa katika "ziwa la moto," ishara ya **maangamizi kamili na ya milele**. Hivyo, mfumo wa Mpinga Kristo utaangamizwa kabisa milele.

Uharibifu huu mkubwa wa mifumo ya Mpinga Kristo ya **Babeli—mama na mabinti**—utalifikisha dunia kwenye kilele cha wakati wa dhiki kuu:


*"Katika kusikiwa kwa habari ya kutekwa kwa Babeli, dunia itatetemeka, na kilio chake kitasikika kati ya mataifa."* (Yeremia 50:33)

Mfumo huu wa Mpinga Kristo hujifanya kana kwamba ni wa Kristo. Unadai kuwa ni Ufalme wa Kristo duniani kabla ya kuja kwake kwa mara ya pili (Mathayo 25:31); umejaa mafundisho ya uongo na makosa; husababisha uharibifu kwa kweli ya Mungu na watumishi wake (Ufunuo 17:6); na ni uumbaji wa Shetani kwa madhumuni ya kuwadanganya makanisa na kuyaweka katika giza totoro. Kwa hakika, huu ni "**siri ya kuasi**."

Leo hii, Waprotestanti huwaita Wakatoliki kuwa ni Mpinga Kristo, na Wakatoliki nao huwataja Waprotestanti kuwa ni Mpinga Kristo. Wote ni sahihi, kwa kuwa wote ni sehemu ya mfumo mmoja mkuu wa Mpinga Kristo ulioelezwa katika Biblia.

Twamshukuru Bwana kwa kutufunulia macho yetu ili kutambua kweli hii kuu.

**AMENI**



*Kwa Masomo zaidi Tuandikie Ujumbe kupitia:*

*Email: thekingdom1_6@gmail.com au isayaruhala25@gmail.com*

*©HAKIUZWI*

***Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482***